

**SHIRIKA LA FEDHA LA KIMATAIFA**  
**IDARA YA MAMBO YA NJE**  
**WASHINGTON DC**  
**20431 USA**

Taarifa kwa Vyombo Vya Habari

31 Machi 2009

**UJUMBE WA IMF WATOA WITO KWA TANZANIA KUTOA**  
**VICHOCHEO VYA KUKUZA UCHUMI**

Ujumbe wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ukiongozwa na Bwana Roger Nord uliotembelea Tanzania kuanzia tarehe 17 hadi 31 Machi, 2009, kwa lengo la kufanya tathmini ya uchumi kwa mujibu wa mashauriano yaliyofanyika chini ya Kanuni za IMF (Article IV Consultation) na tathimini ya tano ya mpango wa ushauri kwa nchi zinazoendelea juu ya Sera za kukuza uchumi (Policy support Instrument- PSI). Ujumbe ulikutana na Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Mkulo; Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Prof. Benno Ndulu; Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Fedha na Uchumi ya Bunge la Muungano, Mheshimiwa Dk. Abdalla Kigoda (MB), Mwenyekiti wa Kamati ya Mahesabu ya Mashirika ya Umma ya Bunge la Muungano, Mheshimiwa John Cheyo (MB); Viongozi Waandamizi wa Serikali; wawakilishi toka sekta binafsi na wajumbe toka taasisi zisizo za kiserikali.

Mwishoni mwa ziara yake leo, Bwana Roger Nord, mkuu wa ujumbe huo kwa Tanzania, ametoa taarifa ifuatayo hapa Dar es Salaam:

“Baada ya kipindi cha muongo mmoja wa mafanikio makubwa katika uchumi, mtikisiko wa sekta ya fedha duniani umeleta changamoto ngumu kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Uchumi unategemewa kukua kwa kiwango cha asilimia mbili (2%) mwaka 2009, toka kiwango cha asilimia tano (5%) mwaka jana, kabla ya kuanza kuimarika taratibu mwaka 2010. Kuimarika huku kutategemea hatua thabiti za kuimarisha mifumo ya fedha katika nchi zilizoendelea ili kuchochea mahitaji bidhaa katika uchumi.

“Tanzania itaathirika pia. Ujumbe wa IMF unakadiria ukuaji wa uchumi wa nchi kufikia kati ya asilimia nne hadi tano (4-5%) kwa mwaka 2009 ukilinganishwa na kadirio la ukuaji wa asilimia saba na nusu (7½) mwaka jana. Sekta za kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya mauzo ya nje ikiwa ni pamoja na sekta ya utalii zitaathirika kutokana na kushuka kwa mahitaji katika soko la dunia na hata mahali pengine kutokana na bei za bidhaa kushuka sana. Uwekezaji wa moja kwa moja toka nje ambao umeendelea kuwa chanzo muhimu cha ukuaji wa uchumi hapa Tanzania, utashuka kwa vile wawekezaji wa kimataifa huenda wakapunguza vitega uchumi au wataahirisha mipango yao ya kuwekeza”.

“Katika kipindi cha muda mfupi ujao, ujumbe wa IMF unaona kuna kiwango fulani cha kuchochea uchumi. Sera nzuri za mapato na matumizi katika miaka ya hivi karibuni zimetoa mwanya wa kupanua nakisi ya bajeti ya mwaka 2008/09 kiwango cha asilimia tatu (3%) ya pato la taifa. Vichocheo zaidi vinatarajiwa katika bajeti ya mwaka 2009/10 inayo andaliwa hivi sasa. Ingawa kiwango cha mfumuko wa bei kiko juu kwa

sasa, IMF inatarajia mfumuko wa bei kuanza kupungua kutokana na bei za vyakula kuanza kushuka katika miezi ijayo. Kwa hiyo ujumbe unaona kuna nafasi ya kulegeza sera ya fedha katika siku zijazo.

“Hata hivyo hatua za muda mfupi za kuchochea ukuaji wa uchumi hazitakiwi kuathiri jitihada za kuleta utulivu katika kipindi cha muda wa kati kwani utulivu huo ni muhimu sana kwa nchi ya Tanzania ili iendelee na ukuaji madhubuti wa uchumi na kupiga hatua zaidi katika juhudi za kupunguza umaskini. Katika muda wa kati ujao sera ya mapato na matumizi ya serikali inatakiwa kuzingatia haja ya kuendelea kudhibiti ongezeko la madeni ya nchi na kuimarisha matumizi ya fedha za umma.

Ni muhimu kuhakikisha kuwa ongezeko la matumizi ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu linakuwa endelevu ili kusaidia kukuza uwezo wa Tanzania kuimarisha ukuaji wa uchumi. Ni vema pia sera ya fedha kuendelea kuandaliwa na kutekelezwa kwa kuzingatia lengo la Benki Kuu ya Tanzania la kudhibiti mfumuko wa bei. Pia mfumo madhubuti na mpana zaidi utahitajika ili kuhakikisha kuwa sekta binafsi inapata uwezo wa kuwekeza na kutoa nafasi za ajira. Ni muhimu vile vile kuimarisha utaratibu wa usimamizi wa vyombo vya fedha ikiwa ni pamoja na sekta ya mifuko ya pensheni ambayo inakua kwa kasi kubwa.

“Inatarajiwa kwamba Bodi ya Utendaji ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF Executive Board) itajadili mashauriano haya ya mwaka 2009 na tathmini ya tano chini ya mpango wa PSI baadaye mwezi Mei, 2009.